Kifo Na Mbingu
(Death And Heaven)

Na

Ellis P. Forsman

Kifo Na Mbingu

Na

Ellis P. Forsman

Octoba 11, 2011

Kifo Na Mbingu

Heb. 9:27

Ili kufika mbinguni, mji wa nafsi zenye haki, ni lazima mtu aende kwa njia ya kifo. Hakuna njia ya mkato.

Kifo ni ahadi ya lazima. Heb. 9:27, "*Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu;*"

Kimsingi maisha ya dunia hii yamejawa na ahadi nyingi, lakini ahadi nyingi hizo hazijatimizwa. Hataivyo hakuna ahadi katika dunia hii ambayo kila mtu anayezaliwa anapaswa kuitimiza. Sio swala la kuisahau; lakini pia sio swala la kuchagua. "*...wanavyowekewa watu kufa....*"

Wakati wa kufa haijulikani. 1 Sam. 20:3, "*...lakini ni kweli aishivyo BWANA, na iishivyo roho yako, iko hatua moja tu kati ya mimi na mauti.*"

Hata kama mtu anaishi katika dunia hii kwa siku moja, au miaka mia moja, kuna hatua moja tu katika chumba cha mauti.

Kifo kinaweza kuwa ya kutisha, lakini pia inaweza kuwa nzuri. Kwa mwana wa Mungu mwaminifu, kifo ni zoezi la mahafali, na hitimisho ya yaliyopita na mwanzo wa umilele usio na mwisho wa furaha, amani na furaha isiyo kifani.

Ujumla Ya Kifo

Kifo ni cha ulimwengu mzima. Kila saa ya kila siku kifo kila wakati hutuzunguka.

Uthibitisho wa kifo kiasili wakati fulani huja ikiwa nzuri. Tunda zuri la ua huweza kuchanua katika ua zuri kwa akisi nzuri na harufu ya kuvutia ing'arishayo hewa, lakini bado na yenyewe hunyauka na kufa.

Mtu anapaswa tu kuendesha gari katika milima iliyo na maporomoko ili kuona uzuri wa rangi wa mamilioni ya majani ya miti inayokufa, kila moja ikionyesha rangi nzuri, na kiujumla ikionyesha umashuhuri wa usanii wa Mungu.

Hunyauka Kama Jani

Mara nyingi, viungo vyote vya mti haviishi kwa mara moja. Kila jani ya kila mti hufa kwa kiwango tofauti; hata rangi.

Zingine hunyauka na kufa wakati wa masika wakati zingine hustawi.

Zingine hufa wakati wa kiangazi kukiwa na upepo mkali au ukosefu wa mvua.

Mengine hunyauka na kuanguka wakati wa vuli wakati joto limeshuka.

Tangazo la nabii wa Mungu lilikuwa na uthabiti kiasi gani katika Isaya 64:6: "*...sisi sote twanyauka kama jani;...*"

Watoto wengi wachanga hutolewa wakiwa bado tumboni wakiwa bado hupendwa, kabla bado hawajachanua katika ujana. Au baadhi ya vijana wadogo wa kiume na wa kike hunyauka kabla ya wakati wao wa vuli katika maisha yao.

Majani huanguka chini kimyakimya.

Moja kwa moja hupoteza rangi na kuanguka, lakini kwa hakika hakuna mtu anayeweza kuelezea maendeleo ya maisha yao na kifo kwanzia mwanzo hadi mwisho.

Ndivyo ilivyo kwa binadamu. Sio muda mrefu mwanadamu ameanza kuishi anapoanza kufa.

Wengi wetu hufikiri kifo ni kuwa mbali zaidi, lakini haiku hivyo. Mtu anaanza kufa pale anapoanza kuishi.

Kifo kama tunavyoifikiria, ni hatua moja kutoka sehemu ambapo mtu anaweza kukanyaga katika dunia hii katika hatua za umilele.

Mtu anapoondoka katika dunia hii, anaacha mwili wake wa nyama.

Nafsi yake isiyoharibika utoka katika mwili wake uharibikao na siku Fulani ita "*vaa isiyoharibika.*" 1 Kor. 15:54-55, "*Basi huu uharibikao utakapovaa kutokuharbika, na huu wa kufa utakapovaa kutokufa hapo ndipo litakapo kuwa lile neon lililoandikwa, mauti imemezwa kwa kushinda. Kuwapi, ewe mauti kushinda kwako? U wapi ewe mauti uchungu wako?*

Roho Ya Mwanadamu Haifi

Mwanzo kabisa, Biblia inasema Mungu alipuliza pumzi ya uzima ndani ya mwanadamu na mwanadamu akawa "*nafsi hai*".

Taraja la mbinguni linaweza kuwa halina maana kama roho ya mwanadamu itakufa. Yoh. 11: 26, "*Naye kila aishiye na kuniamini hatakufa...*"

Mwili huu tulionao hauku kusudiwa kuwa sehemu ya makazi ya jumla ya nafsi. Roho itakaa milele aidha mbinguni au motoni.

Mbingu

Mbinguni ni sehemu iliyoahaidiwa na Yesu. Yohana 14:2-3, "*Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo ningaliwaambia, maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali; nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi nanyi mwepo.*"

Yesu hakuishi kwenye nyumba alipokuwa anaishi duniani. Mat. 8:20, "*Yesu akamwambia, mbweha wana pango na ndege wa angani wana viota, lakini Mwana wa Adamu hana pa kulaza kichwa chake.*"

Lakini jengo lililobuniwa na kujengwa na mbunifu wa mbinguni itakuwa kamilifu kwa furaha, amani, na furaha ya watu wa Mungu.

Mbingu ni sehemu iliyo na uzuri isiyolinganishwa. Hakuna sehemu katika dunia hii iliyozeeka ambayo inaweza kulingana na uzuri wa mbinguni. Ufu. 21:1-22:6, "*Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza, simekwisha kupita, wala hapana bahari tena. Nami nikauona mji ule mtakatifu Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari kama bibi arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe. Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, tazama maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake, naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. Naye atafuta kila chozi katiaka macho yao, wala mauti haitakuwapo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa maana mambo ya kwanza yamekwisha kupita. Na yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi akasema, tazama nayafanya yote kuwa mapya. Akaniambia andika ya kwamba maneno hayo ni amini na kweli. Akaniambia imekwisha kuwa. Mimi ni Alfa na Omega, Mwanzo na mwisho. Mimi nitampa yeye mwenye kiu, ya chemchemi ya maji ya uzima bure. Yeye ashindaye atayarithi haya, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu. Basi waoga na wasioamini, na wachukizao na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili. Akaja mmoja wa wale malaika saba waliokuwa na vile vitasa saba vilivyojaa yale mapigo saba ya mwisho, naye akanena nami akisema njoo huku nami nitakuonyesha yule bibi arusi Mke wa Mwana Kondoo. Akanichukua katika Roho mpaka mlima mkubwa, mrefu, akanionyesha ule mji mtakatifu Yerusalemu, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mwenyezi Mungu; weenie utukufu wa Mungu na mwangaza wake ulikuwa*

mfano wa kito chenye thamani nyingi kama kito cha yaspi, safi kama bilauri; ulikuwa na ukuta mkubwa, mrefu nwenye milango kumi na miwili, na katika ile milango malaika kumi na wawili; na majina yameandikwa ambayo ni majina ya kabila kumi na mbili za Waisraeli. Upande wa mashariki milango mitatu, na upande wa kaskazini milango mitatu, na upande wa kaskazini milango mitatu, na upande wa magharibi milango miatatu. Na ukuta wa mji ulikuwa na misingi kumi na miwili, na katika ile misingi majina kumi na mawili ya wale mitume kumi na wawili ya Mwana Kondoo. Na yeye aliyesema name alikuwa na mwanzi wa dhahabu, apate kuupima huo mji, na milango yake, na ukuta wake. Na ule mji ni wa mraba, na marefu yake sawasawa na mapana yake. Akaipima mji kwa ule mwanzi; ulikuwa kama maili elfu na mia tano; marefu yake na mapana yake, na kwenda juu kwake ni sawasawa. Akaupima ukata wake ukapata dhiraa mia na arobaini na nne, kwa kipimo cha kibinadamu, maana yake cha malaika. Na majenzi ya ukuta ule yalikuwa ya yaspi, na mji ule ulikuwa wa dhahabu safi, mfano wa kioo safi. Na misingi ya ukuta wa mji ulikuwa umepambwa kwa vito vya thamani vya kila namna. Msingi wa kwanza ulikuwa yaspi; wa pili yakuti samawi; wa tatu kalkedoni; wan ne zumaridi; wa tano sardoniki; wa sita akiki; wa saba krisolitho; wa nane zabarajadi; wa kenda yakuti ya manjano; wa kumi krisopraso; wa kumi na moja hiakintho; wa kumi na mbili amethisto. Na mji ule hauhitaji jua wala mwezi kuuangaza, kwa maana utukufu wa Mungu huutia nuru, na taa yake ni Mwana Kondoo. Na mataifa watatembea katika nuru yake. Na wafalme wa nchi huleta utukufu wao ndani yake. Na milango yake haitafungwa kamwe mchana; kwa maana humo hamna usiku. Nao wataleta utukufu na heshima ya mataifa ndani yake. Na ndani yake hakitaingia kamwe chochote kilicho kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo na uongo, bali wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana Kondoo. Kasha akaniambia maneno haya nia amini na kweli. Naye Bwana, Mungu war oho za manabii, alimtuma malaika wake kuwaonyesha watumwa wake mambo ambayo hayana budi kuwako upesi."

Uvuvio Wa Kimbingu

Matukio mengi mazuri ya asili nzuri, iliyoumbwa na Mungu, imewavutia mamilioni ya wasafiri wenzangu katika dunia hii. Bado yote maelezo yote yasiyolinganishwa kwa maneno ya wavumbuzi, ikafunuliwa kwa ndimi za wanenaji, ikapakwa rangi na wachoraji haiwezi kwa hakika kuelezea mbingu.

Umati mkubwa utakuwa pale.

Ufu. 7:9-10, *"Baada ya hayo nikaona na tazama mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, wamesiamama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele za Mwana Kondoo, wamevikwa navazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao; wana matawi ya mitende mikononi mwao; wakilia kwa sauti kuu wakisemaWokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana Kondoo.*

Hitimisho

Nakuuliza, je unataka kwenda mbinguni? Kama mbingu siyo makazi yako, basi jehanamu itakuwa. Mimi napanga kwenda mbinguni, wewe je? Mtu anaendaje mbinguni?

Mtu ni lazima afanyike Mkristo ili hilo lifanyike? Zifuatazo ni hatua muhimu zinazomfanya mtu awe Mkristo:

- **Imani.** Waeb. 11:6, *"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao."* Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na mimi akniambia kwamba haamini kwamba Mungu yuko. Kwa vile nilisha batizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu mandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba Mungu yuko. Lakini ili kuwa upande salama, labda anapaswa kwenda kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani atampeleka mbinguni (kama kuna mbingu), na si motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Matend. 2:38, *"Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* Matend 11:18, *"...Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima."* Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "Kwamba kuna mwizi!" taratibu unachukua simu ya mkononi, unawapigia polisi. Kidogo polisi wanafika na kumshika mwizi. Alafu anapiga kelele, "samahani;

samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Toba iliyokweli ni kwamba mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloleta badiliko la matendo. Tunatakiwa kufanya hivyo kabla hatujawa wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10, *"Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."* Tuna kiri nini? Kwamba tuna amini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

  Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekeza kwenye kitu Fulani; si kwamba mtu ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kuitimiza haki yote, *"Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni mwanangu mpendwa, ninaye pendezwa naye."* (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo sahihi la kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, "*Imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote."* Tuna batizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, si kwa sababu ni haki yetu.

  Kwa kweli, tusipo batizwa, tungali katika dhambi zetu. *"Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matend. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? "*Kwa ajili ya ondoleo la dhambi*". Kwa nini watu wanapenda kuach hatua inayotuondoa dhambi zetu?

  Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. *"Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili*

*kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu iki hiki, "*Unakawilia nini? Simama, na ubatizwe, na uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko, *"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale umekufa. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake. Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlvyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika katika mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusiitumikie dhambi tena."* (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumiwa na damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru na dhambi zetu za zamani kama tu tukibatizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuwezi kupeleka maiti makaburini, na kumwekea udongo kidogo juu yake; tunauzika mwili.

Kama hujafanyika Mkristo, kwa nini usizingatie leo?